FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

# Sura ya Kumi

# Njia za maambukizi ya VVU


Katika sura hii utajifunza njia za maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU).

Jamii yetu imekumbwa na janga la UKIMWI. UKIMWI ni kifupisho cha Upungufu wa Kinga Mwilini. UKIMWI husababishwa na VVU. VVU vinakaa kwenye majimaji ya mwili wa binadamu, majimaji ya vidonda na damu.

## Njia za maambukizi ya VVU

### (a) Kuchangia vifaa kama sindano, wembe, mkasi na mswaki.

Tazama picha hizi kisha soma maelezo yanayofuata.



**Kielelezo namba 1** Vifaa vinavyochangia maambukizi ya VVU



SAYANSI STD 3 (05/07/2021).indd 92 8/5/21 4:04 PM


FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Picha inaonesha vifaa vyenye ncha kali kama sindano ya hospitali, sindano ya kushonea nguo na mkasi. Vilevile, inaonesha mswaki. Kuchangia vifaa vyenye ncha kali na mtu mwenye VVU kunaweza kusababisha maambukizi.

Vifaa vyenye ncha kali vitumike kwa uangalifu na usahihi. Vilevile, kuchangia mswaki na mtu mwenye VVU kunaweza kusababisha maambukizi ya VVU. Unashauriwa usichangie vifaa hivi katika matumizi ili kuepuka maambukizi ya VVU.

### (b) Kuongezewa damu yenye VVU

Chunguza picha hii, kisha soma maelezo yanayofuata.



**Kielelezo namba 2** Kumwongezea damu mgonjwa



SAYANSI STD 3 (05/07/2021).indd 93 8/5/21 4:04 PM

FOR ONLINE USE ONLY

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

Picha hii inaonesha mgonjwa aliyelazwa hospitalini akiwa ametundikiwa chupa ya damu. Damu ni lazima ipimwe kwa umakini ili kuhakikisha haina vimelea vya VVU. Mgonjwa anapaswa kuongezewa damu safi na salama.

### (c) Maambukizi kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto

Mtoto anaweza kupata VVU kutoka kwa mama aliyeambukizwa VVU wakati wa kujifungua. Vilevile, mtoto anaweza kupata VVU kutoka kwa mama wakati wa kunyonya.

### (d) Kufanya ngono au kubakwa na mtu aliyeambukizwa VVU

Kufanya ngono na mtu mwenye VVU husababisha maambukizi ya VVU. Pia watoto wadogo wanaweza kupata maambukizo wakibakwa na watu wenye VVU. Hivyo wanatakiwa kuwa waangalifu wasidanganywe na kulazimishwa kufanya ngono. Vilevile, wasipite na kucheza maeneo hatarishi yenye vishawishi vya kubakwa. Maeneo hayo ni kama vile vilabu vya pombe na kumbi za starehe. Pia vibanda vya kuoneshea sinema. Ni muhimu kutoa taarifa kwa wazazi endapo mtu yeyote ataonesha dalili za kutaka kukufanyia vitendo vya ngono.

FOR ONLINE USE ONLY



SAYANSI STD 3 (05/07/2021).indd 94 8/5/21 4:04 PM

Tukumbuke kuwa UKIMWI ni hatari na hauna chanjo wala tiba. Huwezi kumtambua mtu mwenye VVU kwa kumtazama hadi apime. Kwa hiyo, ni muhimu kutambua njia za maambukizi ya VVU na namna ya kujikinga.

FOR ONLINE USE ONLY
DO NOT DUPLICATE

## Zoezi

**Jibu maswali yafuatayo:**

1. Taja njia zinazochangia maambukizi ya VVU unazozifahamu.
2. Eleza kwa namna gani vifaa vyenye ncha kali vinachangia maambukizi ya VVU.
3. Andika kirefu cha VVU na UKIMWI.

FOR ONLINE USE ONLY



SAYANSI STD 3 (05/07/2021).indd 95
8/5/21 4:04 PM